**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**

Simu: +255 26 2324455
FAX: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mow.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P. 2888,
**40470 DODOMA.**
TANZANIA

**DODOMA**

**27 Januari, 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

Wizara ya Ujenzi inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa inayosambaa katika mitandao ya kijamii ikionesha wananchi wakipita katika Daraja la muda la JP Magufuli (Kigongo – Busisi) mara baada ya vivuko vya MV Mwanza, MV. Misungwi na MV. Sengerema Mkoani Mwanza kusimama kutoa huduma kutokana na changamoto ya magugu maji katika eneo hilo hali iliyoathiri utendaji kazi wa mifumo ya uendeshaji wa vivuko hivyo.

Kufuatia changamoto hiyo, Uongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), walifanya utaratibu wa kuhakikisha wananchi hao wanavuka kwa usalama katika daraja la muda kutokana na ujenzi unaoendelea wa Daraja hilo ambapo Kamati ya Usalama ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Sengerema walisimamia zoezi hilo kwa umakini.

Aidha, Maafisa wa Polisi walijipanga kila baada ya mita mia moja (m100) ili kuhakikisha usalama wa wananchi na utaratibu mzuri wa uvukaji unazingatiwa bila ya kuathiri miundombinu ya Daraja la JP Magufuli na wananchi hawakuvunja geti kama inavyosemekana kwenye video hizo.

Hadi sasa, TEMESA imefanikiwa kurejesha vivuko viwili kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma katika eneo hilo na hivyo, Wizara ya Ujenzi inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kuwa watulivu na kushirikiana na mamlaka husika ili kuhakikisha zoezi la kuvuka linaendelea kwa usalama na utulivu pale ambapo changamoto kama hizo zinajitokeza.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutoa fedha kwa wakati ili kuhakikisha Daraja hilo ambalo limefikia asilimia 96.3 linakamilika ili kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa.

Imetolewa na;

Abdallah H. Ulega (Mb)
**Waziri wa Ujenzi**